# HIFADHI YA TAIFA
# TARANGIRE

*Kiswahili*



***"Paradiso ya Tembo"***

2019/1




## *Karibu Hifadhi ya Taifa Tarangire!*

**Karibu Hifadhi ya Taifa Tarangire! Tunayo furaha kuwa na wewe hapa na tunashukuru kwa kutuamini na kuja kututembelea. Kuhakikisha mahitaji yako yanafikiwa ni jukumu letu kwa sababu mteja kwetu ni mfalme. Haijalishi unakuja kutembelea hifadhi kwa matembezi ya siku au zaidi, hifadhi hii ina vivutio vingi ambavyo vitamfurahisha kila mmoja.**

**Hifadhi hii ni ya kipekee nchini yenye idadi kubwa ya tembo wanaoonekana kwenye makundi makubwa na pia ni eneo lenye ndege wengi kwa ukanda huu wa Afrika Mashariki. Hifadhi pia ina uoto wa asili wa miti aina ya Migunga na Mibuyu ambayo hufanya hifadhi kuwa na mandhari nzuri. Fanya safari yako iwe ya kipekee maishani kwa kupanga safari na kuja kutembelea hifadhi hii ambayo ina mchanganyiko wa vivutio ambavyo havipatikani mahali pengine Tanzania.**

# Historia ya Hifadhi

Jina Tarangire lilitokana na mto mkuu unaopita ndani ya hifadhi ambao unaitwa Mto Tarangire. Mto huu umeanzia maeneo ya nyanda za juu za mto kondoa upatikanao katika Mkoa wa Dodoma na kupita katikati ya Hifadhi hii. Hifadhi hii ilianzishwa mwaka 1970 ikiwa na ukubwa wa kilometa za mraba 2,850.




# Jinsi ya kufika hifadhini

Hifadhi ya Taifa Tarangire inafikika kwa njia ya barabara na anga.

**Kwa Anga**: Hifadhi inafikika kupitia kiwanja cha kimataifa cha Kilimanjaro (km 46 hadi Arusha) na ndege za kukodi toka kiwanja cha ndege Arusha na kwenye kiwanja cha Kuro kilichopo ndani ya Hifadhi.



**Kwa Barabara:** Hifadhi ipo umbali wa km 121 kutoka jiji la Arusha hadi lango kuu la kuingia hifadhini kupitia barabara ya Arusha - Babati.

# Hali ya Hewa

Hifadhi ya Taifa Tarangire inaweza kutembelewa kwa kipindi chote cha mwaka japokuwa wakati mzuri zaidi wa kutembelea hifadhi hii ni kuanzia mwezi Juni hadi Septemba na kuanzia Desemba hadi mwanzoni mwa mwezi Machi. Kipindi cha mvua za muda mfupi ni kuanzia mwezi Oktoba hadi Novemba na kipindi cha mvua nyingi ni kuanzia mwezi Machi hadi Mei. Kwa msimu wa kiangazi joto hufika hadi nyuzi 38 za sentigredi na kipindi cha baridi joto hufika nyuzi 15 za sentigredi.

# Vivutio vilivyopo

Hifadhi ina vivutio vingi vya utalii kuanzia aina mbalimbali za wanyama wanaopatikana kwenye nyika na kwenye ardhi oevu zilizopo.

- **Wanyamapori**

  Hifadhi hii inafahamika kama eneo la kitalii kutokana na uwepo wa idadi kubwa ya wanyamapori. Kuna makundi makubwa ya wanyama wanaovutiwa na kuwepo kwa mto Tarangire na ardhi oevu. Wanyama wanaoonekana kwa wingi ni tembo, nyati,

twiga, nyumbu, pofu, pundamilia, simba, duma na fisi. Pia hifadhi inakupa fursa ya kuona makundi makubwa ya nguchiro wanaoishi kwenye vichuguu vya mchwa na hii inaifanya safari yako kuwa ya kipekee kabisa.

- **Uoto wa asili wa Miti ya Mibuyu**

  Hifadhi hii imetawaliwa na uoto wa asili wa savana ambao una miti mingi na mikubwa ya mibuyu inayoipa hifadhi mwonekano wa kipekee kabisa. Kama miti hii ingekuwa na uwezo wa kuongea basi isingekuwa na haraka kwani kwa mwonekano wake kuna mambo mengi ya kujifunza ikiwa ni pamoja na umri mkubwa wa hadi miaka 3,000 na kuwa na kipenyo cha hadi futi 100. Ni miti iliyoishi duniani kwa kipindi cha muda mrefu.

- **Mto Tarangire**

  Mto Tarangire hupata maji yake kutoka kwenye mito ya misimu inayopatikana Mashariki na Kusini Mashariki mwa hifadhi. Mto huu hutiririsha maji yake kupitia hifadhini kwa upande wa Kaskazini na kumwaga kwenye ziwa Burunge. Ndani ya hifadhi mto huu unaungana na ardhi oevu za Silale, Gurusi na Larmakau. Mto huu ndio chanzo pekee cha maji kwa kipindi cha kiangazi hivyo kusababisha kuwepo kwa mkusanyiko mkubwa wa wanyama na hii hutoa fursa nzuri kwa utalii wa kuangalia wanyama.

- **Uwepo wa aina nyingi za ndege**

  Hifadhi hii inatoa fursa ya kuweza kuona makundi makubwa ya ndege wenye rangi za kuvutia. Ndege zaidi ya aina 550 wameainishwa wakiwa katika makazi yao ya asili ya ardhi kavu na maeneo yenye maji. Kwa kawaida idadi kubwa huonekana





maeneo yenye uoto wa miti ya migunga, ardhi oevu na mto Tarangire. Wakati wa kufanya utalii utaweza kuona ndege kama mbuni, tai, tumbusi, ndege karani, korongo domowazi, korongo domokijiko na korongo-taji, kusi kijivu, kwaru, kasuku, tetere, kweche na wengine wengi

- **Vichuguu vyenye kuipamba ardhi ya Hifadhi**

Vichuguu vya mchwa vinavyopatikana hifadhini ni kivutio kingine kinachopatikana katika hifadhi ya Taifa Tarangire ambapo watalii watafurahia kuona na kutembelea kwani vichuguu hivi vimetengenezwa na mchwa kwa udongo uliochanganywa na mate yao.  Pia ni makazi ya wanyama wa aina mbalimbali kama vile nguchiro-dumavu, kakakuona, nyoka na mhanga pindi vinapoachwa.



# Shughuli za Utalii

- **Utalii wa kutwa wa kuona wanyama kwa kutumia gari**

Aina hii ya utalii itamwezesha mtalii kuona wanyama wa aina mbalimbali akiwa ndani ya gari. Hifadhi hii ina makundi makubwa ya wanyama kama vile tembo, nyati, twiga, choroa, tandala mdogo, swala granti, swala tomi, kongoni, nyumbu, simba, chui, fisi na chatu wapandao miti. Utalii huu kwa kawaida hufanyika nyakati za asubuhi na jioni kwa sababu hali ya hewa ni nzuri na ni nyakati za wanyama kujitafutia mahitaji yao hasa chakula. Utalii huu unampa mtalii fursa ya kuona wanyama wawindao wakifanya mawindo yao na kuifanya siku yake kuwa ya kipekee kabisa.

- **Matembezi ya miguu**

Aina hii ya utalii unampa mtalii elimu zaidi ya mazingira ya asili na wanyama kwani unamwezesha kutembea hifadhini huku akitazama wanyama kwa karibu zaidi. Utalii huu pia hufanyika zaidi nyakati za asubuhi na jioni na humpatia mtalii vionjo na uzoefu tofauti wa safari.

- **Utalii wa kutazama ndege**

Hifadhi ina aina zaidi ya 550 za ndege ambapo kunaifanya kuwa eneo la kipekee kabisa kwa wageni wanaopenda kutazama ndege. Mtalii anapokuwa kwenye utalii huu asikose kuangalia makundi makubwa adimu ya ndege kama kwaru-shingonjano, korobindo mkiamwekundu na kusi kijivu ambao hupatikana Tanzania tu.





- **Utalii wa kuruka kwa puto**

  Utalii huu huwapa wageni nafasi ya kuingalia hifadhi kwa sura tofauti. Kuangalia wanyama na mandhari kutokea juu huleta ladha tofauti. Hebu jaribu kufikiria ukiwa unaruka juu ya mto Tarangire huku jua likiwa limemulika nyasi na kuonekana kwa rangi ya dhahabu huku nyika zikiwa zimepambwa na miti mikubwa ya mibuyu, huku tembo na wanyama wengine wakiwa wamejikusanya pembezoni mwa mto Tarangire, vyote hivi vinaifanya safari ya mtalii iwe ya kuvutia sana!.

- **Utalii wa picha na filamu**

  Hifadhi hii ni eneo zuri kwa utalii wa kupiga picha na filamu kutokana na mandhari nzuri iliyopo. Mchanganyiko wa nyika, mto Tarangire, ardhi eovu, miti ya mibuyu, makundi ya wanyama kama tembo, twiga na nyati na ndege hutoa fursa ya kipekee kwa ajili ya kutengeneza filamu.

- **Utalii wa usiku wa kuona wanyama kwa kutumia gari**

  Utalii huu hufanyika nyakati za usiku ambapo mtalii ataweza kuiona hifadhi kwa jicho tofauti na mchana. Kwa watalii wanaopenda kuona wanyama watembeao usiku na wale wasioonekana mchana kwa urahisi kama vile chui, nungunungu, paka mwitu, fungo na mhanga, aina hii ya utalii inatoa fursa ya kuwaona wanyama hawa wakiwa wanajitafutia chakula usiku.

# Malazi

Hifadhi ina aina mbalimbali za malazi ikiwa ni pamoja na kambi za jumuiya na maalum, koteji hosteli na nyumba ya kupumzikia. Pia zipo aina mbalimbali za malazi ndani na nje ya hifadhi zinazomilikiwa na watu binafsi

# TOZO

| | | *Waafrika Mashariki Tshs* | *Wasio wa Afrika Mashariki US $* | *Wasio wa Afrika Mashariki waishio Tanzania US $* |
|---|---|---|---|---|
| **A.** | **Tozo ya Uhifadhi kwa mtu kwa siku** | | | |
| i. | Umri wa miaka 16 na zaidi | 10,000 | 45 | 22.5 |
| ii. | Umri kati ya miaka 5 hadi 15 | 2,000 | 15 | 7.5 |
| iii. | Children below the age of 5 years | Free | Free | Free |
| **B.** | **Kupiga kambi - Kambi za jumuiya** | | | |
| i. | Umri wa miaka 16 na zaidi | 5,000 | 30 | 30 |
| ii. | Umri kati ya miaka 5 hadi 15 | 2,500 | 5 | 5 |
| iii. | Children below the age of 5 years | Free | Free | Free |
| **C.** | **Kupiga kambi - Maeneo maalum** | | | |
| i. | Umri wa miaka 16 na zaidi | 10,000 | 50 | 50 |
| ii. | Umri kati ya miaka 5 hadi 15 | 5,000 | 10 | 10 |
| iii. | Children below the age of 5 years | Free | Free | Free |
| **D.** | **Kupiga kambi - Muda maalum** | | | |
| i. | Umri wa miaka 16 na zaidi | 15,000 | 50 | 50 |
| ii. | Umri kati ya miaka 5 hadi 15 | 5,000 | 10 | 10 |
| iii. | Children below the age of 5 years | Free | Free | Free |
| **E.** | **Kupiga mahema – Kambi za kuhama (Fly Camping)** | | | |
| i. | Umri wa miaka 16 na zaidi | 5,000 | 50 | 50 |
| ii. | Umri kati ya miaka 5 hadi 15 | 2,500 | 10 | 10 |
| **F.** | **Utalii wa Matembezi kwa miguu** | | | |
| i. | Matembezi ya muda mfupi(saa 1 hadi 4) kwa watu wazima | 5,000 | 20 | 20 |
| ii. | Matembezi ya muda mfupi kwa watoto wenye umri zaidi ya miaka 12 | 2,500 | 10 | 10 |
| iii. | Matembezi ya muda mrefu (zaidi ya masaa 4) kwa watu wazima | 10,000 | 25 | 25 |
| iv. | Matembezi ya muda mrefu kwa watoto wenye umri zaidi ya miaka 12 | 5,000 | 15 | 15 |
| **G.** | **Tozo kwa ajili ya mwongoza mgeni/askari kwa kundi** | | | |
| | Ada ya uongozaji | 5,000 | 20 | 20 |
| **H.** | **Tozo ya kulala hoteli ndani ya hifadhi (Concession Fees)** | | | |
| i. | Umri wa miaka 16 na zaidi | 30,000 | 40 | 40 |
| ii. | Umri kati ya miaka 5 hadi 15 | 10,000 | 10 | 10 |

**I. Tozo za malazi** (kwa mtu mmoja kwa siku)

*Mawasiliano na hifadhi yafanyike kabla*

| | | | |
|---|---|---|---|
| i. Nyumba ya kupumzika wageni | 20,000 | 30 | 30 |
| ii. Hosteli | 5,000 | 10 | 10 |

**J. Tozo ya utalii wa usiku**

| | | | |
|---|---|---|---|
| i. Mtu mzima | 10,000 | 50 | 50 |
| ii. Mtoto | 5,000 | 25 | 25 |

**K. Kurekodi video kwa kundi la watu 2-20**

Hii ni kwa wanaorekodi video za matumizi binafsi (muziki au maigizo)

| | | | |
|---|---|---|---|
| i. Ndani ya Hifadhi (hulipwa tofauti na tozo nyingine kwa siku) | 100,000 | 100 | 100 |
| ii. Viwanja vya Ofisi za Makao Makuu | 100,000 | 50 | 50 |

**L. Tozo za magari**

| | *Usajili Tanzania TShs.* | *Usajili Kigeni US$.* |
|---|---|---|
| i. Uzito hadi kilo 2000 | 20,000 | 40 |
| ii. Uzito kilo 2,001 hadi 3,000 | 35,000 | 150 |
| iii. Uzito kilo 3001 hadi 7,000 | 60,000 | 200 |
| iv. Uzito kilo 7001 hadi 10000 | 150,000 | 300 |
| v. Uzito zaidi ya tani 10 (ruhusa toka kwa Kamishna Uhifadhi) | 300,000 | 500 |

vi. Magari ya wazi yatatozwa asilimia 50 zaidi ya tozo za kawaida

**M. Faini kwa kusababisha ajali** TShs. 200,000

**N. Faini kwa kuzidisha mwendo**
(aina zote za magari) Tshs. 50,000

**O. Tozo kwa yenye usajili wa Tanzania (Magari/boti/trela na ndege zinazopaki ndani ya Hifadhi kwa mwaka)**

| | |
|---|---|
| i. Uzito hadi kilo 2000 | 50,000 |
| ii. Uzito kati ya kilo 2,001 hadi 3,000 | 100,000 |
| iii. Uzito kati ya kilo 7001 hadi 10,000 | 200,000 |
| iv. Trekta, trela na boti | 50,000 |
| v. Ndege | 200,000 |

| **P. Tozo za kutua kwa ndege** | **Ndege za Nje (US $)** | | **Ndege za ndani (TShs)** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Binafsi** | **Biashara** | **Binafsi** | **Biashara** |
| a) Hadi siti 4 | 50 | 120 | 10,000 | 15,000 |
| b) Siti 5 - 12 | 120 | 170 | 15,000 | 20,000 |
| c) Siti 13 - 20 | 170 | 320 | 20,000 | 35,000 |
| d) Zaidi ya siti 20 | NA | NA | 50,000 | 60,000 |

**Q. Kurekodi filamu kwa siu kwa mtu**

Gharama hizi zinajumuisha tozo ya uhifadhi, kupiga kambi na kurekodi filamu ambayo inajumuisha mataifa yote — US $ 250

**R. Tozo kwa makundi ya wanafunzi au binafsi**

| | |
|---|---|
| i. Tozo ya Uhifadhi kwa shule za msingi, sekondari na kidato cha 5&6 | TShs 2,000 |
| ii. Tozo ya uhifadhi kwa vyuo na vyuo vikuu | TShs 5,000 |
| iii. Tozo ya kupiga kambi kwa shule za msingi, sekondari na kidato cha 5&6 | TShs 2,000 |
| iv. Tozo ya kupiga kambi kwa vyuo na vyuo vikuu | TShs 3,000 |
| v. Malazi ya nyumba na hosteli kwa wanafunzi | TShs 5,000 |

**S. Pasi ya Mkurugenzi kwa mwaka** — US $ 100

*(Yahitaji ruhusa toka kwa Kamishna Uhifadhi)*

**U. Utalii wa Puto** (Kwa mtu mmoja kwa safari moja) — US $ 40

**T. Kuingia zaidi ya Mara Moja kwa Siku Hifadhini (Multiple Entry)**

Kutakuwa na uwezekano wa kuingia zaidi ya mara moja hifadhini ambapo tozo husika za hifadhi zitalipwa. Kutakuwa na aina mbili za ruhusa ya kuingia mara zaidi ya moja;

i. Kibali cha siku ambacho kina uhalali wa masaa kumi na mbili ya mchana na kinachoruhusu kuingia mara zaidi ya moja ndani ya muda halali wa kibali hicho

ii. Kibali cha hifadhi ambacho kina uhalali wa masaa ishirini nne na kilichoruhusu kuingia zaidi ya mara moja Hifadhini ndani ya muda halali ulio kwenye kibali hicho

**U. Tozo ya kupewa eneo la uwekezaji na ada ya kukodisha Ardhi kwa mwaka**

(Tozo hizi hazirejeshwi kwa wawekezaji wapya watakaowekeza ndani ya Hifadhi za Taifa)

| | |
|---|---|
| i. Tozo ya kupewa eneo la uwekezaji (hairejeshwi) | US$ 5,000 |
| ii. Tozo ya Mwaka inayoendana na ukodishaji wa Ardi: | |
| a) Kambi za Msimu | US$ 1,000 |
| b) Kambi za hema za kudumu (PTC) | US$ 10,000 |
| c) Loji | US$ 20,000 |

**ZINGATIA:**

- Tozo ya kiingilio cha hifadhi na gari inaweza kutumika zaidi ya mara moja ndani ya muda wa kibali (multiple entry);
- Fedha ikilipwa hairudishwi;
- Uhakiki wa utambulisho langoni ni lazima;
- Tozo zote hazijajumuisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT);
- Raia Mkaazi wa Tanzania na wategemezi wao wanaoishi hapa Tanzania lazima wawe na vielelezo vifuatavyo; Kibali cha Ukaazi daraja A, B au C, Hati ya msamaha, Pasi ya muda ikiwa imeambatishwa na risiti ya malipo ya serikali na barua ya kukiri, na Pasipoti ya kidiplomasia au kitambulisho;
- Wakazi wa Jumuia ya Afrika Mashariki inamaanisha wale wenye utaifa wa nchi za Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda na Sudani ya Kusini;
- Wenye Utaifa wa Jumuia ya Afrika Mashariki inamaanisha mbali na Tanzania ni lazima waonyeshe hati zao za kusafiria kwenye malango ya kuingilia hifadhini;
- Magari binafsi toka nchi nyingene za Jumuia ya Afrika Mashariki hayaruhusiwi kufanya biashara ya utalii ndani ya hifadhi; na
- Kwa utalii wa kufanya video wasiliana na Uongozi wa hifadhi kwa ajili ya kupata mwongozo na msaada.





# Tembelea Hifadhi

*Tembelea hifadhi na onja yaliyo kwenye tamaduni za kiafrika ambapo wazawa hushirikisha mila na tamaduni zao ambapo utaweza kuboresha maisha ya wenyeji kwenye ulimwengu huu wa mabadiliko. Ahsante!*

# Sheria na Taratibu za Hifadhi

**Uwapo ndani ya Hifadhi hairuhusiwi**

- Kusumbua wanyama na ndege
- Kupiga kilele kama kupiga honi za magari, muziki kwa sauti kubwa au usumbufu mwingine wowote kwa wageni wengine
- Kung'oa, kuchuma, kukata au kuharibu mimea
- Kutupa taka, vichungi vya sigara au njiti za kiberiti
- Kusababisha moto hifadhini
- Kuingiza wanyama wafugwao
- Kuendesha mwendokasi zaidi ya kilomita 50 kwa saa
- Kuendesha nje yaa barabara na sehemu zisizoruhusiwa
- Kuingia na silaha ya aina yeyote ndani ya Hifadhi

**Kumbuka**

Kuwa ndani ya hifadhi kabla ya saa 12:00 asubuhi na baada ya saa 12:00 jioni ni kosa, isipokuwa kwenye maeneo ya kulala wageni yanayotambulika.




**Kwa mawasiliano zaidi:**
Mkuu wa Hifadhi
Hifadhi ya Taifa Tarangire,
S. L. P. 3134
**Arusha - Tanzania**

**Simu:** +255 739 222 685, +255 766 536 139 / +255 689 062 248
**Barua pepe:** tnp@tanzaniaparks.go.tz
**Facebook:** Tarangire National Park-Hifadhi ya Taifa Tarangire
**Twitter:** @tarangirepark
**Instagram:** tarangire_national_park
**Tovuti:** www.tanzaniaparks.go.tz